Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
**Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

# ELIMU Bulletin

JARIDA LA MTANDAONI: Toleo Na.34 - 2024

wizara_elimuTanzania wizara_elimuTz www.facebook/moestvt.com www.wyestu.blogspot.com www.moe.go.tz ELIMUTZ

*Tunaboresha Elimu Yetu*

## TOLEO MAALUM

## Miaka Mitatu Safari ya Mageuzi katika Elimu





## - KAZI IENDELEE -

MIAKA 3 YA RAIS SAMIA KAZINI




# Baadhi ya Dondoo za Mafanikio ya Awamu ya Sita


**Ongezeko la Bajeti Sekta ya Elimu**




**Mikopo ya Wanafunzi Elimu ya Juu**




**Wanufaika wa Mikopo ya Elimu ya Juu**




## Kuondoa tozo 6% na adhabu 10%

kwa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu

## 1,122

Idadi ya wanufaika wa Samia Skolaship

**Vyuo vya VETA katika kila Mkoa na Wilaya**

**Tuzo za Watafiti waliochapisha katika majarida ya kimataifa**

**Ujenzi wa Kampasi mpya 14 za vyuo vikuu katika Mikoa 14**

**Mapitio ya Sera na Mitaala Mipya**



MIAKA 3 YA **RAIS SAMIA KAZINI**

# Mapinduzi Makubwa ya Sera, Mitaala na Miundombinu ya Elimu



Miaka mitatu madarakani ya Rais Dk Samia Suluhu Hassan madarakani imeleta mapinduzi makubwa katika sekta ya elimu nchini kwa kuwezesha upatikanaji wa sera na mitaala mipya ya elimu inayolenga kuongeza ujuzi, ubunifu na uwezo wa kujiajiri kwa wahitimu wa elimu nchini.

Serikali ya Awamu ya Sita pia imetoa kipaumbele katika Sekta ya Elimu kwa kuhakikisha mindombinu ya shule za msingi na sekondari imeboreshwa ili kila mtoto wa Kitanzania apewe nafasi ya kupatiwa elimu bora na ya uhakika.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof Adolf Mkenda amesema uwepo wa sera na mitaala mipya ambayo utekelezaji wake umeanza Januari 2024 utaleta mageuzi makubwa katika sekta ya elimu nchini katika ngazi zote yaani, Elimu ya Awali, Elimumsingi, Sekondari, Ualimu, Elimu ya Kati na Elimu ya Juu.

Serikali imekamilisha Mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na kuandaa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 toleo la 2023 na Mitaala ya elimu ngazi ya elimu ya awali, msingi, sekondari na elimu ya ualimu ambapo utekelezaji wake umeanza Januari 2024.

Sera iliyoboreshwa na mitaala imelenga kuwa na wahitimu wenye; maarifa, mwelekeo, maadili na ujuzi unaoakisi mahitaji sasa na ya baadaye katika maendeleo ya Taifa na kuweza kushindana na kushiriki kikamilifu katika soko la ajira duniani.

Kwa muda mrefu imeonekana haja ya kuboresha sera na mitaala kwani ili kuwapatia wahitumu elimu ujuzi na maarifa ambapo mapitio hayo yamezingatia masuala muhimu yanayopewa kipaumbele katika dunia yakiwemo mabadiliko ya tabianchi, Elimu kuhusu Uraia wa Dunia (Global Citizenship Education) na Stadi za Karne ya 21.

Serikali imefanya maboresho kwenye baadhi ya maeneo katika Sera ya Elimu na Mafunzo ili kutoa elimu ya ujuzi badala ya elimu ya taaluma pekee ambapo elimu ya lazima itakuwa ya miaka 10 badala ya saba kama ilivyo sasa.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alitoa taarifa Bungeni juu ya adhima ya serikali kuhakikisha utekelezaji wa maboresho hayo ambayo yataenda kwa awamu sambamba na kufuta mtihani wa darasa la saba na badala yake kuanza kufanyika kwa tathmini darasa la sita kwa ajili ya kujiunga na elimu ya lazima ya sekondari.

Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya uongozi wa Rais Dk Samia Suluhu Hassan ulilfikia hatua hiyo baada ya kubainika kwa changamoto mbalimbali zikiwemo, mfu-



# MIAKA 3 YA RAIS SAMIA KAZINI




mo wa elimu kujikita zaidi kwenye elimu ya jumla na kukosa fursa za elimu na mafunzo kwa kuzingatia mahitaji na njia mbalimbali za ujifunzaji kutokidhi kulingana na mazingira.

"Mitaala kutokidhi mahitaji ya mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, kisayansi na kiteknolojia, mfumo usio fanisi wa udhibiti na ithibati ya elimu na upungufu wa nguvu kazi. Changamoto hizo zilizaa hitaji la kuboresha sera yetu ya elimu ili kukidhi mahitaji ya sasa na wakati ujao."Alisema Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa

Maeneo kadhaa yameboreshwa ikilinganishwa na sera iliyopita kwa kuongeza fursa za elimu ya amali (elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi) ambayo itaanza kutolewa kuanzia kidato cha kwanza.

Elimu ya ualimu nayo itaanza kuanza kutolewa kwa wahitimu waliomaliza kidato cha sita na kuendelea. Mafunzo ya ualimu yatajumuisha mwaka mmoja wa mafunzo chini ya uangalizi (internship) baada ya kuhitimu mafunzo tarajali (Pre-service training).

Pia, Mfumo wa upimaji na tathmini sasa utazingatia mahiri zinazohitajika kwa kila ngazi kwa lengo la kuwa na upimaji endelevu na matumizi ya mbinu mbalimbali za upimaji na tathmini ya maendeleo ya wanafunzi katika kujifunza.

"Serikali itatoa na kusimamia matumizi ya kitabu kimoja cha kiada kwa kila somo katika elimu ya msingi na Sekondari ili kufanikisha upimaji wa matokeo ya ufundishaji na ujifunzaji unaofanana pia Serikali itaweka utaratibu wa kubaini na kuendeleza wanafunzi wenye vipaji na vipawa mbalimbali."





MIAKA 3 YA RAIS SAMIA KAZINI

# Serikali imewekeza ili kuongeza fursa kwa Elimu ya Juu nchini



Ongezeko la udahili, fursa za mikopo , uendelezaji wa kitaaluma kwa wahadhiri nchini na uboreshaji wa miundombinu imekuwa ni agenda ya Serikali ya awamu ya Sita kuimarisha mchango wa Elimu ya Juu katika kuleta maendeleo nchini.

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk Samia Suluhu Hassan katika kipindi chake cha miaka mitatu madarakani imewekeza ili kuongeza fursa kwa Elimu ya Juu katika agenda ya maendeleo nchini.

Katika kuimarisha mchango wa Elimu ya Juu, Serikali imekuwa ikitekeleza miradi mbalimbali katika agenda ya maendeleo ikiwemo Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (Higher Education for EconomicTransformation - HEET).

Kupitia mradi wa HEET, Serikali mwezi Mei 27, 2021 Serikali imewezesha upatikanaji wa mkopo nafuu wenye thamani ya Dola za Kimarekani Milioni 425 sawa na Shilingi bilioni 972.0 kutoka Benki ya Dunia.

Hali hiyo imeongeza fursa za upatikanaji wa Elimu ya Juu ambapo vyuo vikuu 14 vya umma nanTaasisi zinazosimamia Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia zinanufaika na mradi huo wa HEET.

Baadhi ya Taasisi zilinufaika na mradi wa HEET ni pamoja na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU).

Kupitia mradi wa miaka mitano, HEET, Serikali itajenga mabweni 34,vyumba vya mihadhara na madarasa 130, kumbi za mikutano ya kisayansi 23, maabara/karakana za kufundishia 108, miundombinu ya shambani na vituo atamizi 10 kwa ajili ya kwa kuendeleza ubunifu na kukarabati miundombinu mbalimbali .

Maboresho hayo yanatarajiwa kuongeza idadi ya wanafunzi wanaosoma programu za kipaumbele (STEM) kutoka wanafunzi 40,000 kwa mwaka 2020 hadi kufikia 106,000 mwaka 2026.

Mradi pia unalenga kuboresha mitaala ya programu za kipaumbele cha Taifa kwa kuhuisha na kuandaa mitaala mipya zaidi ya 290 ili kuifanya iendane na mahitaji ya soko la ajira ndani na nje ya nchi.

Hadi kufikia mwezi Januari, 2024 Taasisi za elimu ya juu 19 zimeanza mchakato wa kuandaa mtaala unaoendana na soko la ajira ambapo Taasisi 12 zimekusanya taarifa za wahitimu(Tracer study) na taasisi tisa (9) zimekamilisha tathmini ya mahitaji ya soko la ajira (need assessment).

Aidha, Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi umewezesha taasisi sita (6) kufanya tathmini ya uwezo wa ndani wa taasisi( self assessment) na kuwezesha taasisi za elimu ya juu 19 kuanzisha Kamati za Ushauri wa Kitasnia (Industrial Advisory Committees) kwa lengo la kutoa ushauri wa kitasinia wakati wa uandaaji wa mitaala mipya.

Mradi huu wa unatarajia kusomesha Wahadhiri 387 (wanawake 235, wanaume 152) katika shahada za uzamivu (PhD) na Wahadhiri 444 (wanawake 274, wanaume 270) katika shahada za umahiri (MSc) na mafunzo ya muda mfupi.

Hadi kufikia mwezi Januari, 2024 jumla ya wahadhiri na watumishi 342 wamewezeshwa kuhudhuria masomo ndani na nje ya nchi ambapo watumishi 230



# MIAKA 3 YA RAIS SAMIA KAZINI

(wanaume 156 na wanawake 74) wanahudhuria masomo ya Uzamivu na watumishi 112 (wanaume 77 na wanawake 35) masomo ya Uzamili.

Aidha, imewezesha mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 1,692 katika masuala mbalimbali ambapo wahadhiri 27 (20 Uzamivu na 7 Uzamili) kutoka vyuo vikuu binafsi katika fani za sayansi, teknolojia na Hesabu pia wamenufaika na ufadhili huo.

Ili kuimarisha mifumo ya usimamizi wa Elimu ya Juu na kuratibu na kuzijengea uwezo wa ubunifu Taasisi za Elimu ya Juu, Sayansi, Teknolojia na ubunifu kwa na kufanya mapitio ya sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ya Elimu ya Juu, Sayansi, Teknolojia na Ubunifu iende na wakati.

Hadi kufikia mwezi Januari, 2024 taasisi ya Elimu za Juu na sekta binafsi zimewezeshwa kuingia mikataba ya ushirikiano ambapo mikataba ya makubaliano 112 imesainiwa.

Aidha, imewajengea uwezo wahadhiri pamoja na watumishi wa taasisi za elimu ya juu kuhusu umuhimu wa ushirikiano na sekta binafsi pamoja na viwanda katika utoaji wa mafunzo na tafiti za kisayansi.

Mradi wa HEET pia umewezesha ujenzi wa Kampasi za Vyuo Vikuu katika Mikoa ya Pembezoni ambapo Serikali ya Awamu ya Sita imelenga kukuza uchumi na kuboresha huduma za jamii kwa uwiano sawia katika mikoa na maeneo yote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kutokana na azima hiyo ya serikali, katika kutekeleza mradi wa HEET, inaendelea na ujenzi wa Kampasi 14 mikoa ya pembezoni ikiwemo: Kigoma, Ruvuma, Singida, Mwanza, Kagera, Tanga,Mwanza, Tabora, Manyara, Simiyu, Shinyanga, Lindi, Rukwa, na Katavi.

Nia ya Serikali ni kuongeza taasisi zinazotoa ujuzi na mafunzo ya ufundi katika mikoa isiyo na taasisi za Elimu ya Juu na kuongeza fursa za elimu ya juu katika mikoa ya pembezoni.

Katika kufanikisha hilo, Serikali ya Awamu ya Sita imejenga mazingira/fursa za kiuchumi ,kupanua nafasi za elimu ya ufundi, ujuzi na stadi za Maisha kupitia vyuo vitakavyojengwa maeneo ya pembezoni.

Lengo pia ni kuongeza fursa za ajira mbalimbali katika mikoa ya pembezoni na hivyo kukuza uchumi na hali za maisha ya jamii katika maeneo yatakayonufaika na utekelezaji wa mradi wa HEET.



Ujenzi wa miundombinu mbalimbali kama kujenga miundombarabara, shule, vituo vya afya, maji, umeme zitakazojengwa zitarahisisha uendeshaji wa taasisi zaelimu zitakazojengwa kwenye mikoa ya pembezoni.

Serikali imeendelea kuimarisha mchango wa tafiti za taasisi za Elimu ya Juu, kuongeza bajeti ya mikopo ya wanafunzi .

Ongezeko la mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu kumeongoza fursa kwa kuwawezesha wanafunzi wa Tanzania wenye uhitaji na stahiki ya kupata mkopo kwa ajili ya elimu ya juu.

Serikali ya awamu ya sita imeongeza bajeti ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kutoka Shilingi bilioni 464 mwaka 2020/21 hadi Shilingi bilioni 786 mwaka 2023/24.

Ongezeko hili la Bajeti limewezesha kuongeza wanufaika wa mkopo kutoka wanafunzi 142,170 mwaka 2020/21 hadi wanafunzi 220,278 mwaka 2023/24 na pia imeondoa tozo ya asilimia 6 ya kulinda thamani ya fedha katika urejeshaji wa mkopo iliyokuwa inatozwa kwa wanufaika wa mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.

Aidha, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu imeondoa tozo ya adhabu ya asilimia 10 ya mkopo ambayo inatozwa kwa wanufaika waliochelewakulipa mikopo hiyo na imezindua huduma ya mikopo ya elimu inayotolewa na Benki ya NMB kwa ajili ya wanafunzi wa Elimu ya Juu.

Hii ni katika kufikisha adhima ya Serikali ya Awamu ya Sita kuhakikisha kila mwanafunzi mwenye kustahili kupata elimu ya juu haikosi kwa kigezo cha kukosa mkopo.

Katika kuhakikisha kuwa nchi inaenda sambamba na sayansi na teknolojia , Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilianzisha Programu ya Mama Samia Skolashipu ili kuongeza idadi ya wahitimu wa elimu ya juu wa fani ya sayansi.

Serikali imeendelea kuongeza idadi ya wahitimu wa fani za sayani katika elimu ya juu kwa kuongeza fursa za upatikanaji wa Elimu ya Juu kwa wanafunzi waliofaulu vizuri Kidato cha Sita katika michepuo ya sayansi na kufadhiliwa na Programu ya Samia Skolaship iliyoanzishwa 2022 ambapo jumla wa wanafunzi1,122 wananufaika.



MIAKA 3 YA RAIS SAMIA KAZINI

# Uwekezaji Mkubwa katika Elimu ya Amali kuzalisha Wahitimu wenye ujuzi na Umahiri



Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk Samia Suluhu Hassan imejipambanua kwa kuhakikisha inaweka msisitizo katika Elimu ya Amali nchini lengo ni kuhakikisha kuwa wanafunzi wanaomaliza shule wanakuwa na ujuzi, ubunifu na kuweza kujitegemea.

Hili limejidhihirisha wazi katika Sera ya Elimu, ambapo mfumo wa elimu utajikita katika kujenga umahiri, kupata ujuzi, maarifa, weledi, mwelekeo, mitazamo chanya, maadili na tabia kulingana na mahitaji ya taifa na ulimwengu wa kazi.

Sera ya Elimu iliyoanza kutelekezwa Januari 2024, inaonesha kuwa muundo katika mfumo rasmi wa elimu na mafunzo utakuwa na mwaka mmoja wa elimu ya awali, miaka sita ya elimu ya msingi, miaka minne ya elimu ya sekondari ngazi ya chini, miaka miwili ya elimu ya sekondari ngazi ya juu au miaka mitatu ya amali sanifu na miaka isiyopungua mitatu ya elimu ya juu.

Katika miaka mitatu ya Rais Dr Samia Suluhu Hassan imewekeza katika kuhakikisha kuwa elimu ya amali inatekelezeka kwa kuwekeza katika ujenzi vya vyuo vya ufundi na miundombinu wezeshi kwa wanafunzi nchini.

Na hili liko pia katika sera ya elimu inaonesha kuwa elimu ya sekondari ngazi ya chini itagawanyika katika mikondo miwili ambayo ni mkondo wa elimu ya jumla na mkondo wa elimu ya amali.

Aidha, elimu ya amali itakuwa sehemu muhimu ya mfumo wa elimu na itatolewa kulingana na mitaala

Elimu ya sekondari ngazi ya juu au elimu ya amali sanifu itakuwa hitaji la msingi kwa ajili ya kujiunga na elimu ya juu. Pia elimu ya juu itakuwa baada ya elimu ya sekondari na itagawanyika katika mkondo wa elimu ya jumla na elimu ya amali.

Serikali pia katika kutambua umuhimu wa elimu ya amali , elimu nje ya mfumo rasmi inatambuliwa na watakaopitia mfumo huo watakuwa na fursa ya kujiunga na mfumo rasmi wa elimu kulingana na vigezo vitakavyowekwa.

Serikali ya awamu ya Sita, imeongeza fursa za mafunzo ya amali (Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi) kupitia Vyuo vya Ufundi Stadi-(VET)

Katika kuhakikisha fursa za upatikanaji wa elimu ya amali Serikali ndani ya miaka mitatu ya Rais Dk Samia Suluhu Hassan Madarakani imekalisha ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya Wilaya 25 kupitiaMpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na



# MIAKA 3 YA RAIS SAMIA KAZINI

Mapambano Dhidi ya UVIKO 19 (TCRP).

Vilevile, Serikali inaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa Vyuo vinne vya VETA ngazi ya Mkoa Geita, Njombe, Simiyu na Rukwa ambayo ilikuwa haina vyuo vya ngazi hiyo, ambapo ujenzi umefikia zaidi ya asilimia 97.

Pia imewezesha ukarabati wa vyuo 10 vya VETA ambavyo ni: Ileje, Urambo, Nkasi, Newala, Muleba, Itilima, Babati, Kilindi, Ngorongoro na Kasulu;

Katika mwaka wa fedha 2022/23, Serikali imeanza ujenzi wa Vyuo 64 vya VETA ngazi ya Wilaya katika wilaya ambazo hazina vyuo vya ngazi hiyo pamoja na kuanza kwa ujenzi wa Chuo cha VETA ngazi ya Mkoa katika Mkoa wa Songwe ambao hauna chuo katika ngazi hiyo.

Kwa kuwa elimu ya amali inahitaji walimu mahiri, Serikali imeongeza fursa za elimu ya Ualimu wa Amali ili kuendana na mwelekeo wa Sera iliyoboreshwa ya Elimu na Mafunzo nchini kwa kuimarisha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika Chuo cha Ualimu wa Ufundi Stadi Morogoro.

Katika kufikia azma hiyo, Serikali imewezesha ujenzi wa Hosteli yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 96 kwa wakati mmoja na jumla ya Shilingi milioni 446,921,958.7 zimetumika.

Ili kutoa wigo mpana zaidi ya wananchi kujiunga na mafunzo ya amali, Serikali imeongeza fursa za Mafunzo ya Amali kupitia Vyuo vya Maendeleo ya wananchi (FDC)

Katika kuongeza fursa za mafunzo ya amali kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs), Serikali imekarabati na kuvipatia vifaa vyuo vyote 54 hivyo kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 6,693 mwaka 2015 hadi 16,457 mwaka 2021/22.

Azma hiyo imefikiwa baada ya Serikali kutumia Shilingi bilioni 6.8 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia kwa lengo la kuimarisha ujifunzaji kwa vitendo.

Katika kuongeza fursa za elimu ya ufundi kwa lengo la kuongeza nguvu kazi ya watu wenye ujuzi (skills) katika taifa, Serikali inaendelea na ujenzi wa Chuo cha Ufundi Dodoma ulioanza 28 Mei, 2021.

Awamu ya kwanza ikikamilika, Chuo hicho kitakuwa na uwezo wa kudahili wanafunzi 3,000 kwa mwaka ambapo ujenzi utagharimu Shilingi bilioni 17.9. Ujenzi umefikia katika hatua ya ukamilishwaji ikiwa ni asilimia 99.5;

Zaidi ya hayo Serikali imeandaa mwongozo wa mafunzo unaozingatia ujuzi (Trainingmanual on CBET Curricula Development/Review, Delivery and Assessment).

Aidha, imeandaa Kiunzi cha Mafunzo ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (TEVT Quality Assurance Handbook) kwa ajili ya kuongeza ubora wa mafunzo katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi.

Kupitia mkopo nafuu wenye thamani ya Shilingi bilioni 191.0 kutoka Benki ya Dunia, Serikali imewezesha kuanza kwa utekelezaji wa Mradi wa Elimu ya kujenga ujuzi Afrika Mashariki (East Africa Skills For Transformation And Regional Integration Project - EASTRIP) unaishirikisha pia nchi za Ethiopia na Kenya





MIAKA 3 YA RAIS SAMIA KAZINI

# Maboresho ya Miundominu katika Taasisi za Elimu nchini



*Maktaba ya Chuo cha Ualimu Shinyanga*



*Nyumba za Walimu shule ya Sekondari Dodoma City*



*shule ya Msingi ya Mfano Lukuledi*



MIAKA 3 YA **RAIS SAMIA KAZINI**

# Vifaa vya Kufundishia ikiwemo vya Maabara, Ufundi









MIAKA 3 YA **RAIS SAMIA KAZINI**

# Serikali imeboresha mazingira utoaji elimu jumuishi na kuongeza nafasi za mafunzo kwa wenye mahitaji maalum

Katika kuhakikisha kuwa hakuna mtoto wa Kitanzania anaachwa nyuma katika kupata haki ya elimu, Serikali ya Awamu ya Sita imeboresha mazingira ya utoaji wa elimu jumuishi na kuongeza nafasi za mafunzo kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Katika kutekeleza hilo kwa vitendo, Serikali imehakikisha kuwa fursa za elimu zinatolewa kwa watoto wote wa Kitanzania bila vikwazo lengo likiwa ni kutekeleza falsafa ya "No one is left behind".

Elimu Maalum ni moja ya maeneo ambayo Serikali imekuwa ikiyatilia mkazo kwa kuhakikisha kuwa kuna walimu, miundombinu wezeshi na vifaa vya kujifunzia kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Katika kufikia azma hiyo, Serikali imekamilisha ujenzi wa shule jumuishi ya mfano ya Lukuledi iliyopo Masasi Mkoani Mtwara yenye uwezo wa kuchukuawanafunzi 620 pamoja na Shule Maalum ya Sekondari Patandi – Mkoani Arusha yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 360.

Hizo zote ni jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk Samia Suluhu Hassan ambapo pia inaendelea na ujenzi wa Shule Jumuishi ya Mfano Awali, Msingi na Sekondari Mbuye- Mkoani

Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi hawa wanakuwa na mazingira mazuri ya kujifunzia, serikali imewezesha uchapaji wa vitabu vya wanafunzi wenye mahitaji maalum (wasioona na uoni hafifu) katika ngazi zote za Elimu.

Imewezesha uchapaji wa vitabu vya Braile na Maandishi yaliyokuzwa nakala 6,060 kwa ajili ya wanafunzi wa awali, imechapa vitabu vya Braile na maandishi yaliyokuzwa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum wanaosoma darasa la I-VII.

Kwa upande wa Shule za Sekondari, jumla ya vitabu 9,178 kwa wanafunzi 353 wasioona na vitabu 93,366 kwa ajili ya wanafunzi 3,591wenye uoni hafifu.





***Mmoja wa wanafunzi wenye mahitaji maalum akitumia Kifaa Saidizi kinachokuza maandishi kumwezesha kusoma***




# MIAKA 3 YA RAIS SAMIA KAZINI

Aidha, Serikali pia imewezesha ununuzi wa vifaa saidizi kwa wanafunzi 486 wenye mahitaji maalum wa Elimu ya Juu katika taasisi 11 za umma pamoja na kusambaza vifaa vya kielimu na saidizi kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu wa viungo vikiwemo Vitimwendo 1,454 katika shule za msingi na sekondari;

Kwa upande wa wanafunzi viziwi, Serikali imewezesha ununuzi wa vishikwambi (Tablets) 330 vyenye thamani ya Shilingi milioni 134 kwa shule 15 za msingi zinazopokea wanafunzi hao.

Ili kuweza kuwakia wanafunzi wenye mahitaji maalum, Serikali ya Awamu ta Sita ilizindua Mkakati wa Taifa wa Elimu Jumuishi Nchini wa mwaka 2021/2022 - 2025/2026; pamoja na miongozo minne.






Akizindua miongozo hiyo minne, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda alisema inalenga kuboresha utoaji wa elimu kwa watoto wenye mahitaji maalum ikiwamo kuwafuata majumbani.

Miongozo hiyo imekuwa nafasi nzuri ya kuhakikisha kila mtoto wa Kitanzania anapata elimu bila kujali mazingira aliyopo hivyo kuimarisha utoaji wa elimu jumuishi nchini.

Miongozo hiyo italeta mabadiliko chanya miongoni mwa wadau katika kutimiza azma ya serikali ya kuwapatia fursa ya elimu bora wanafunzi wenye mahitaji maalum nchini.

Miongozo hiyo inatoa fursa kwa familia zenye Watoto wenye mahitaji maalum kuhakikisha wanafunzi hao wanapata huduma stahiki ili kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika mchakato mzima wa ujifunzaji.

Prof Mkenda aliwahimiza wazazi kuandikisha Watoto wenye mahitaji maalum shule na wale watakaohitaji huduma ipelekwe majumbani wanapaswa kuasiliana na Wizara ili kuangalia namna ya kufikishiwa huduma hiyo

Sera ya Elimu na Mafunzo ya somo la elimu jumuishi na lugha ya alama ni lazima kwa mtu yeyote anayeandaliwa kuwa mwalimu hapa nchini.

"Jitihada hizi kubwa mnazoziona zinatokana na msimamo wa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan na nyie wote mnajua ni mashahidi maandalizi haya yalianza mapema na kama mnavyofahamu Rais wetu anataka kuhakikisha kila mtoto anakwenda shule,"alisema Prof Mkenda

Pamoja na miundombinu wezeshi na vifaa vya kujifunzia, Serikali inatambua umuhimu wa Walimu kwa Elimu Maalum na kuhakikisha wanaongeza upatikanaji wao ili kukidhi mahitaji.

Hivyo, katika miaka mitatu tangu Rais Dk Samia Suluhu Hassan ameingia madarakani, Serikali imeongeza vyuo viwili vinavyodahili Walimu wa Elimu Maalum (Mpwapwa na Kabanga).

Vyuo hivyo vina uwezo wa kudahili walimu zaidi ya 500 wanaosomea Elimu Maalum na Jumuishi na kuwajengea uwezo wa namna ya kuwafundisha walimu wa Elimu Maalum na jumuishi.



MIAKA 3 YA **RAIS SAMIA KAZINI**

# Serikali imezindua nyaraka muhimu kukabiliana na dharura, majanga







Katika kipindi cha Miaka Mitatu ya Uongozi wa Awamu ya Sita tunashuhudia Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ikifanya tukio kubwa la uzinduzi wa nyaraka muhimu zitakazosaidia katika kudhibiti, kuzuia na kujiandaa kukabiliana na dharura na majanga na ushuhudiwaji wa Zoezi la Utayari Dhidi ya Dharura za Kikemikali na Kimionzi Tanzania

Uzinduzi huo ulifanywa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Machi 14, 2024 Jijini Dar es Salaam ambapo alisema ni azma ya Serikali kuhakikisha usalama wa nchi na mipaka yake dhidi ya majanga mbalimbali unaimarishwa. Hivyo, katika kuteleza azma hiyo, , jitihada mbalimbali zimeendelea kufanywa ili kuhakikisha nchi inajiandaa na kuwa na utayari wa kukabiliana na majanga, maafa na dharura ya aina yoyote.

Waziri Mkuu alizitaja nyaraka hizo kuwa ni Mpango wa Kitaifa wa Maafa ya Kikemikali, Kibaiolojia, Kiradiolojia na Kinyukilia. (CBRN National Action Plan) ambao utasaidia kutoa elimu wakati wa maafa na Mpango wa Kuitikia wakati wa Dharura za Kinyuklia na Kiradiolojia (Radiological and Nuclear Response Plan) ambao utaeleza namna ya kujiandaa.

"Kama mnavyofahamu nchi yetu imebarikiwa kuwa na mazingira mazuri ya kijografia ukiwemo ukanda wa bahari ya Hindi. Ukanda wa bahari umekuwa ukichagiza shughuli nyingi za usafirishaji kwa njia ya meli na kutumia bandari zetu. ambazo zimekuwa lango la biashara kwa Tanzania na mataifa jirani. Mataifa jirani yamekuwa yakitegemea bandari hii katika shughuli za usafirishaji wa bidhaa mbalimbali" amesema Mhe. Kassim Majaliwa.

Ameongeza kuwa bidhaa hizo, zinaweza kuhusisha matukio mabaya ya kikemikali, kibaiolojia, mionzi au hata yale ya kinyuklia na kwa kupitia zoezi hili tunakwenda kujiimarisha. Matokeo hayo yanaweza yakawa ya makusudi au yasiyo ya makusudi, ambapo yanaweza kuathiri







maisha, biashara na mali za wananchi.

Waziri Mkuu amesisitiza kuwa Wizara na taasisi zinazohusika na kutekeleza mipango hiyo, ikiwemo Mpango Kazi wa Kitaifa wa Maafa ya kikemikali, kibaiolojia, kiradiolojia na kinyukilia (CBRN National Action Plan) na Mpango wa Kukabiliana na Dharura za Kinyuklia na Kiradiolojia (Radiological and Nuclear Response Plan) kutoa ushirikiano utakaohitajika katika kutekeleza miongozo hii kwa taasisi na kwamba isiwe ni nyaraka za makabatini tu bali iwe miongozo ya utekelezaji wa hatua thabiti za kuhakikisha tunajenga nchi imara na salama

Waziri Mkuu alisema kuwa a kutokana na ukweli huo, suala la utayari wa kujikinga, kukabiliana na kupunguza majanga ya kikemikali, kibaiolojia, kiradiolojia na kinyuklia na ujenzi wa miundombinu na mazingira wezeshi kwa wataalamu wa ndani kwa lengo la kujenga utayari wakati wote ni muhimu kwa Taifa.

Waziri wa Elimu, Sayansi na a Teknolojia Prof. Adolf Mkenda alieleza kuwa Nyaraka hizo zitatumika kuwa nyaraka ya kitaifa za miongozo inayochukua mtazamo na mahitaji ya taasisi na wizara mbalimbali za Serikali na wadau wengine waliopewa majukumu katika nyanja za kemikali, kibaolojia, radiolojia na nyuklia, lengo kuu ni kuweka mikakati ya pamoja kama taifa ya namna ya kukabiliana na kujikinga na majanga hayo.

Prof. Mkenda amesema kuwa madhumuni ya mafunzo ya utayari ni kuwapa washiriki maarifa na ujuzi wa kukabiliana na vitisho vya kikemikali, kiradiolojia na kinyuklia, na kusaidia juhudi za kuzuia, kujiandaa na kukabiliana na majanga hayo na tukio la Kemikali, Radiolojia na Nyuklia linaweza kutokea kama matokeo ya ajali, vitendo maalum vya kigaidi au kutolewa kwa makusudi kwa kemikali au vyanzo vya kinyuklia, ikiwa ni pamoja na mionzi inayoweza kuleta tishio kwa afya au kwa mazingira.



MIAKA 3 YA RAIS SAMIA KAZINI

# Kishindo Awamu ya Sita: Waliokatisha masomo warejea shuleni

Novemba 24 Mwaka 2021, Rais Samia Suluhu Hassan aliruhusu wanafunzi wanaokatiza masomo kwa sababu mbalimbali ikiwemo ujauzito kurejea shuleni na kuendelea na masomo kwa mfumo rasmi.

Ili kutekeleza hilo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitoa Waraka Namba 3 wa Mwaka 2021 ulioruhusu urejeshwaji wanafunzi waliokatisha masomo katika elimu ya msingi na sekondari kwa sababu mbalimbali. Fursa hii imewezesha wanafunzi waliokatisha masomo kutokana na ujauzito kukamilisha mzunguko wa elimu yao katika mfumo rasmi.

Waraka huo unaendelea kutekelezwa na Serikali kwa mafanikio ambapo moja ya Taasisi inayotekeleza ni Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) ambayo ilianzisha programu maalum chini ya Mradi wa Kuimarisha Elimu ya Sekondari (SEQUIP).

Taasisi hiyo ambayo katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Waraka huo ilifanikiwa kusajili wanafunzi 3,333 na Mwaka wa Pili ilisajili wanafunzi 3,616 na kwa Mwaka huu wa 2024 hadi kufikia Mwezi Machi tayari wanafunzi 9,971 wamesajiliwa na wanaendelea na masomo yao ili kukamilisha mzunguko wa masomo katika Mfumo Rasmi.

Mmoja wa wanufaika wa programu hii Neema Chaula anayesoma katika Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kituo cha Dodoma amemshukuru Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania kwa kuwafuta machozi kutokana na kuwawezesha kutimiza ndoto zao ambazo zilikuwa zimefutika

"Mimi ni Mwanafunzi wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima Dodoma chini ya Mradi wa SEQUIP niliyekatisha masomo, lakini leo niko shule, namshukuru Mama Samia, tupo tuliokatisha masomo kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ujauzito na ugonjwa. Kwa kweli ametufuta machozi na bila shaka tutaupiga mwingi katika mitihani yetu inayokuja" alisema Neema.







MIAKA **3** YA **RAIS SAMIA KAZINI**

# Mafanikio Awamu ya Sita Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Programu ya Jenga Kesho iliyo Bora (BBT) inahakikisha inaendelea kuwapa nafasi vijana kushiriki kwenye kilimo biashara pamoja na kutambua fursa za kilimo kulingana na wakati uliopo.

Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo Bw. Gerald Mweli akiwasilisha maono ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Programu ya BBT kwenye Kongamano la Maadhimisho ya miaka 62 ya Uhuru wa Tanganyika lililoandaliwa na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) kwa kushirikiana na SUA anasema kutokana na mchango wa kilimo kwenye kuchangia malighafi ya viwandani Serikali ya awamu ya sita imejipanga kuhakikisha Programu ya BBT, vijana wake ambao ni asilima 34 ya watanzania wote wanawezeshwa kushiriki katika Sekta ya Kilimo bila kikwazo chochote ambapo Wizara ya Kilimo iliamua kukaa na wadau mbalimbali ili kujadili njia sahihi ya kupiga hatua kwenye kilimo ikiwemo hoja ya elimu, mikopo na masoko kupitia program hiyo.

Jumla ya Vijana 230 Kutoka maeneo mbalimbali ya nchi wakiwemo vijana waliohitimu Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo walifanikiwa kuchaguliwa katika awamu ya kwanza ambao walienda katika sekta ndogo ya kilimo cha pamba wakiwa ni Maafisa Kilimo, Maafisa Kilimo Wasaidizi na Wahandisi Kilimo.

### Matumizi ya Akili Bandia kuboresha kilimo nchini.

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kupitia Mradi wa Mkulima GPT chini ya ufadhili wa 'BILL na MELINDA GATES Foundation' imetoa mafunzo kwa wakulima wadogowadogo wapatao 20 mkoani Morogoro kuhusiana na Mfumo wa Akili Bandia unaotumia lugha ya kiswahili utakaomsaidia mkulima kuweza kupata ushauri kuhusiana na kilimo cha Mahindi kwa wakati husika lakini pia kutatua tatizo kwenye shamba lake bila uwepo wa Afisa Ugani.

Anabainisha hayo Kiongozi wa Mradi huo na Mhadhiri Msaidizi SUA kutoka Idara ya Infomatikia na Teknolojia ya Habari Bi. Theofrida Maginga wakati akizungumza kwenye warsha iliyofanyika mjini Morogoro ambapo alisema Mkulima GPT ni 'Chatbot' inayowasaidia wakulima kupata taarifa ya namna ya kuandaa mashamba vilevile kusimamia mashamba ya kilimo cha mahindi kwa kutumia Akili Bandia (Artificial intelligence).

Kwa Kutumia Akili Bandia ni kwasababu ya ukuaji wa teknolojia hivyo wao kama watafiti kutoka SUA wanaangalia namna mbalimbali ambazo wanaweza wakatumia teknolojia kuwasaidia wakulima katika kufanya shughuli zao za kila siku japokuwa teknolojia inaweza kutumika si kwenye kilimo pekee bali hata kwenye maswala mbalimbali ya kijamii lakini kwa kuanza Mkulima GPT imelenga kuanza na kilimo cha Mahindi na hapo baadae wataangalia na mazao mengine,

Teknolojia hiyo kwa Wakulima ni sehemu ya ukuaji wa teknolojia na wakulima watapata fursa ya kujua namna ya kutumia Mkulima GPT ili waweze kuanza kilimo cha kisasa ambacho kinafanyika si kwa kutumia Matrekta pekee lakini pia hata kutumia Akili bandia katika kufanya shughuli za kila siku kwa Mkoa wa Morogoro lakini pia na Tanzania kwa ujumla.

Naye aliyekuwa Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Uzamili, Utafiti, Uhaulishaji wa Teknolojia na Ushauri wa Kitaalamu ambaye kwa sasa ni Rasi wa Ndaki ya Tiba ya Mifugo na Sayansi za Afya Prof. Esron Karimuribo alisema teknolojia hiyo ni zaidi ya utafiti ni muendelezo wa kuboresha shughuli za Ugani kwa wakulima nchini ambapo Akili Bandia inatumika kusaidia katika kutoa ushauri wa papo kwa papo na kitu kizuri zaidi Utafiti huo umetumia lugha ya watanzania wengi ambayo ni kiswahili lakini pia imetumia ule mfumo wa 'WhatsApp' ambao watu wengi wameuzoea.

Amesema ili kuboresha matokeo makubwa ya kazi hii taasisi na vyombo husika na maswala yote ya Tehama pamoja na habari ikiwemo TCRA, EGA pamoja na Wizara ya Mawasiliano inabidi waione hii kama huduma muhimu kwa Taifa ikiwezekana yawekwe mazingira rafiki kuanzia bei za vifurushi na upatikanaji wa simu za 'WhatsApp' kwa njia rahisi ili wakulima wengi ambao wanahitaji huduma hiyo kuweza kuwa na nyenzo hizo pamoja na uwezo wa kidedha kuweza kupata huduma hiyo kwa haraka zaidi.

### UTAFITI, TEKNOLOJIA NA UCHUMI WA BULUU

***SUA yachangia Utafiti Uliochapishwa katika Jarida la Mazingira***

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kinajivunia Dk. Winfred B. Mbungu, kutoka Idara ya Uhandisi wa Rasilimali za Maji na Maji, Shule ya Uhandisi na Teknolojia, kwa mchango wake mkubwa katika mada kuu ya utafiti katika jarida tukufu la Chakula cha Asili yenye kichwa cha habari 'Makabiliano ya mabadiliko yanayoendeshwa na Wadau yanahitajika kwa usalama wa lishe unaozingatia hali ya hewa katika Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara,'.

Mada hii ni matokeo mashuhuri ya juhudi za uundaji shirikishi wa 'Integrated Future Estimator for Emissions and Diets' (iFEED), sehemu ya Mradi wa Maendeleo ya Kilimo Mahiri wa Hali ya Hewa wa GCFAFRICAP. Inaangazia umuhimu wa kilimo, mabadiliko ya hali ya hewa na usalama wa chakula Kusini mwa Jangwa la Afrika. Mada hiyo inajadili athari za kilimo kinachozingatia





# MIAKA 3 YA RAIS SAMIA KAZINI

mabadiliko ya hali ya hewa katika usalama wa chakula Kusini mwa Jangwa la Afrika, kwa kuangazia nchi za Tanzania, Malawi, Afrika Kusini, na Zambia. Inasisitiza haja ya dharura ya kuongeza uzalishaji wa kilimo ili kujumuisha vyakula vyenye virutubishi vingi zaidi na kupendekeza kuwa kupanua maeneo ya kilimo ni muhimu isipokuwa kuna uboreshaji wa haraka wa mazao. Utafiti pia unachunguza changamoto za mabadiliko haya muhimu, ikiwa ni pamoja na uwezekano wa kuongezeka kwa uzalishaji wa gesi chafuzi na matatizo ya kiuchumi na kisiasa ya kutegemea uagizaji wa chakula kutoka nje.

## Ufumbuzi wa soko la wakulima kidijitali

Wataalam kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) wamegundua mfumo mpya ambao utawawezesha wakulima na wafugaji wa kuku kupata masoko na kuuza kwa njia ya mtandao na kuwafikia watu wengi zaidi kwa urahisi.

Dkt. Sixbert Mourice ambaye ni Mhadhiri Mwandamizi kutoka Idara ya Mimea Vipando na Kilimo Bustani anabainisha kuwa mfugaji ataweza kupakua mfumo huo uliopo kwenye playstore ujulikanao kama E Kuku kwenye simu yake janja ya mkononi na kujiunga kwa ajili ya kuweza kuuza mayai na kuku kwa nchi nzima kwa urahisi. Anasema mfugaji atapaswa kujisajili kwa namba ya simu ambayo imesajiliwa na ataingizwa kwenye mfumo ili aweze kuingiza bidhaa zake, na bidhaa hizo zitadumu kwa saa 24 baada ya huo muda bidhaa zitaondoka, hivyo itampa nafasi ya kuhariri baada ya kila saa 24 hii ni sambamba na kwenda na mabadiliko ya bei ya kila siku.

Hata hivyo kutakuwa na suala la Takwimu hivyo itaonesha bei ya bidhaa kwa kila wilaya ambapo kutakuwa na bei ya juu, bei ya chini, na bei ya wastani hivyo itampelekea mkulima kujua na kuuza bidhaa kwa bei ya usawa na sio kuuza kwa bei ambazo sio za kweli au sio za wakati huo, pia takwimu hizo zitasaidia pia kwenye tafiti mbalimbali.

## Kukuza Uchumi wa Buluu

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, (SUA) kupitia kwa wataalam wake wabobezi wa Elimu ya Viumbe maji, ina mchango mkubwa katika kufanikisha ndoto ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini Rais Dk. Hussein Mwinyi kuwainuia wanachi wa visiwa hivyo kiuchumi kupitia matumizi ya rasimali zilizopo baharini maarufu kama Uchumi wa Buluu.

Mwalimu Nahida Yusufu kutoka shule ya Sekondari ya Wasichana ya Ben Bela iliyopo Unguja Zanzibar, Anasema kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imekuwa na shauku kubwa ya kuwakwamua wananchi kiuchumi kupitia rasilimali za bahari na hivyo kwa kupitia elimu waliyopata SUA, haswa ufugaji wa Samaki kisasa wameona chuo hicho kinatoa elimu ambayo kwa kiasi kikubwa wananchi na hasa wanafunzi wa Zanzibar wanatakiwa kuipata ili kuweza kuelewa namna ya kufaidika na uchumi wa Buluu.

Mwanafunzi Rehema Ali Bushiri akizungumza kwa niaba ya wanafunzi wenzake amesema ziara hiyo imekuwa na manufaa kwao kwa kuwa wamekuwa akiisikia SUA kwa muda mrefu kama Chuo Kikuu cha Kilimo kikongwe nchini lakini sasa wamefahamu chuo kilivyo na wamehamasika kuja kusoma chuoni hapo katika siku zijazo baada ya kuhitimu masomo yao na kufaulu vizuri na hatimae kujiunga SUA kwa masomo ya elimu ya juu.

## MRADI HEET

Mradi huu wenye thamani ya shilingi bilioni 73,600,000,000.00 una lengo la kuongezan udahili wa wanafunzi, kuongeza ubora na kukubalika kwa programu za maeneo ya vipaumbele zinazotolewa katika Vyuo Vikuu vya Umma, pamoja na kuboresha utawala na usimamizi wa Mfumo wa Elimu ya Juu katika Taasisi na katika nchi. Mradi huu unatekelezwa kwa miaka mitano (2021/2022 – 2025/2026) unahusisha upanuzi wa miundombinu, ukarabati, Ununuzi, kuwajengea uwezo wafanyakazi, Uanzishaji wa uboreshaji wa Mitaala, Kuanzisha na kuimarisha uwezo wa kiuvumbuzi na tafiti zenye tija pamoja na Kujenga uwezo wa uzalishaji wa mapato ya ndani.

## Uboreshaji wa mitaala

Wadau mbalimbali wa elimu kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) wameendelea kupitia na kufanya mabadiliko ya mitaala ya elimu ya Chuo itakayotumika kwa ajili ya ufundishaji wa masomo mbalimbali yanayotolewa na Chuo hapo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Seneti inayoshughulika na masuala ya Stadi za Awali Dkt. Damas Philip amesema kuwa lengo la kufanya mapitio ni kuboresha kulingana na hali ya kiuchumi ili uendane na maendeleo ya taifa na pia kuzalisha wahitimu ambao wanakua na stadi bora za kufanya kazi kulingana na fani wanazo somea.

Nae Mwl. Lidya Bupilipili anayefanya kazi katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Huduma kwa Wanafunzi aliongeza kuwa mapitio ya maboresho hayo yatasaidia kuimarisha zaidi wahitimu kulingana na uhitaji wa sasa katika jamii, na kuongeza kuwa masomo kama ya usuluhishaji wa migogoro yatasaidia kutatua migogoro mbalimbali katika jamii wanazoenda kuzihudumia.

Mtaala mpya pia utamuwezesha mwanafunzi wa kila fani anayehitimu kuwa na uwezo wa kujiajiri mwenyewe kuliko kutegemea ajira Serikalini, hata hivyo amesema kuwa kwa wale watakaotaka kupata kazi Serikalini na sekta binafsi watafanya vyema katika ushindani kwenye soko la ajira.

Mapitio hayo ya mitaala yanayoendelea SUA ni muendelezo wa shughuli za uboreshaji wa elimu unaotekelezwa na Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) kwa miaka mitano na kufadhiliwa na Benki ya Dunia.



# Anuani za Taasisi zilizo chini ya Wizara

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU),**
Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S.L.P 6562,
7 Mtaa wa Magogoni,
11479 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2113694, 2113691
Barua Pepe: es@tcu.go.tz

---

Mkurugenzi Mtendaji,
**Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB),**
HESLB House, 1 Mtaa wa Kilimo -TAZARA,
Barabara ya Mandela,
P.O. Box 76068,
15471 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 736 665 533/ 739 665 533
Baruapepe: ed@heslb.go.tz

---

Katibu mtendaji,
**Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA),**
Eneo la Viwanda Mikocheni,
Barabara ya Bagamoyo,
S.L.P 2624 au 32019,
14112 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2700493-6/9 na 22 2772423
Barua Pepe: esnecta@necta.go.tz

---

Mtendaji Mkuu,
**Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTVET),**
S.L.P 17007, DODOMA.
Simu: +255 26 2323 121 / 0733 77 77 51
Barua Pepe: info@nacte.go.tz

---

Mtendaji Mkuu,
**Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM),**
Nunge Street, Old Catholic Church Road,
S.L.P 71, BAGAMOYO, PWANI.
Simu: +255 23 244 0216
Barua Pepe: adem@adem.ac.tz

---

Mkurugenzi Mkuu,
**Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH),**
Barabara ya Ali Hassan Mwinyi,
S.L.P. 4302,
14113 Kijitonyama,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 (022) 2771358/ 2774023/ 2700749
Baruapepe: dg@costech.or.tz

---

Mkurugenzi Mkuu,
**Taasisi ya Elimu Tanzania (TET),**
Plot 132, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P. 35094, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 0735 041168
Barua Pepe: director.general@tie.go.tz

---

Mkurugenzi Mkuu,
**Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA),**
S.L.P 34578,
Mikocheni B, Bima Road,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Barua Pepe: info@tea.or.tz
dg@tea.or.tz

---

Mkurugenzi Mkuu
**VETA Makao Makuu,**
Plot No. 18, Central Business Park (CBP)
Barabara ya VETA,
S.L.P 802,
26 DODOMA.
Simu: +255 26 2963661
Baruapepe: info@veta.go.tz

---

Mtendaji Mkuu,
**Tume ya nguvu za Atomic Tanzania (TAEC)**
S.L.P 743,
23114 Engutoto, Block J, Plot No 216,
ARUSHA
Simu: +255 272 9700054
Barua Pepe:dg@taec.go.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM),**
Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani,
S.L.P. 35091, Mtaa wa Chuo Kikuu
16103 Dar es Salaam
Simu: +255222410700
Baruapepe: vc@udsm.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Ardhi University (ARU),**
Plot No. 3, Observation Hill Blok L,
University Road,
P.O. Box 35176, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 738 357 310-12
Baruapepe: aru@aru.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi, Muhimbili (MUHAS),**
9 Barabara ya Umoja wa Mataifa,
Upanga Magharibi,
S.L.P. 65001,
11103 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2150302-6
Baruapepe: vc@muhas.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA),**
S.L.P 3000,
Barabara ya Edward Moringe, Mtaa wa Kilimo,
01 MOROGORO
Simu: +255 23 260511-4
Barua Pepe: sua@sua.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Mzumbe (MU),**
S.L.P 1, MOROGORO
Simu:
Barua Pepe: mu@mzumbe.ac.tz
info@mzumbe.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),**
S.L.P 259,
Mtaa wa Benjamin Mkapa,
Jengo la Benjamin Mkapa,
41107 DODOMA.
Simu: +255 26 2310001/2/3
Barua Pepe: vc@udom.ac.tz
relations@udom.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT),**
S.L.P. 23409,
14110 Open University Road,
Kinondoni Municipality,
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2668820/ 2668992
Baruapepe: vc@out.ac.tz

---

RASI wa Chuo,
**Chuo Kikuu kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE),**
Taifa Road Next to Benjamin Willium,
S.L.P 2329,
15105 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2850975
Barua Pepe: principal@duce.ac.tz
dpacademic@duce.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ushirika Moshi,**
06 Barabara ya Sokoine Moshi,
S.L.P 474
KILIMANJARO
Simu: +255 272 751 833
Barua Pepe: info@mocu.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kushiriki Cha Elimu Mkwawa (MUCE),**
Mtaa wa Mkwawa Chuo,
S.L.P. 2513,
51111 IRINGA CBD.
Simu: +255 26 2702 751
Baruapepe: principal@muce.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST),**
S.L.P. 131,
Barabara ya 01 MUST,
01 MBEYA.
Simu: +255(0)25 2957542/4
Barua pepe: vc@mustnet.

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NMIST),**
Kampasi ya Tengeru, Barabara ya Nelson Mandela,
S.L.P. 447,
23301 TENGERU, ARUSHA
Simu +255 272970001
Baruapepe: vc@nm-aist.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere,**
S.L.P 976, Butiama, MARA
Simu:
Barua Pepe: info@mjnuat.ac.tz

---

Mkurugenzi
**Bodi ya Huduma za Maktaba (TLSB),**
27 Mtaa wa Bibi Titi Mohamed,
S.L.P 9283
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2150048/9
Barua Pepe: info@tlsb.go.tz

---

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Taifa ya UNESCO,**
7 Magogoni Street,
P. O. Box 20384,
11479 DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2126598/ 22 2134292
Baruapepe: info@natcom.go.tz

---

Mkurugenzi,
**Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)**
23 Mtaa wa Bibi Titi Mohammed,
S.L.P. 20679,
11103 DAR ES SALAAM
Simu:
Baruapepe: info@iae.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ufundi Arusha (ATC),**
Junction of Moshi-Arusha and Nairobi Roads,
P.O. Box 296,
23105 ARUSHA.
Simu: +255 (0) 27-297 0056
Baruapepe: rector@atc.ac.tz/pro@atc.ac.tz

---

Mkurugenzi,
**Kituo cha Maendeleo Dakawa,**
S.L.P 1733,
MOROGORO.

---

Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT),**
Kona ya Bibi Titi na Barabara ya Morogoro
S.L.P 2958
11104 DAR ES SALAAM
Simu:
Barua Pepe: principal@dit.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA),**
30 Barabara ya Kibada,
S.L.P 9193,
17107 Kigamboni,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Baruapepe: rector@mnma.ac.tz